

# »Uzalishaji wa maharage na usimamizi wa baada ya mavuno«

Uzalishaji wa maharagwe ni mdogo kwa sababu ya usimamizi duni wa mazao, rutuba duni ya udongo, wadudu na magonjwa, mbegu zisizo na ubora. Kufuata mbinu sahihi za usimamizi husababisha mavuno mengi.

Wakati wa kupanda maharagwe ni muhimu kupanda mseto ili kuzuia wadudu na magonjwa. Epuka kupalilia wakati wa kuchana maua, ili yasidondoke.

## Kupanda na kusimamia maharagwe

Chagua udongo wenyе rutuba, usio na maji mengi na epuka maeneo yenye changarawe kwa ukuaji mzuri wa mmea.

Chagua mbegu bora za aina moja, na usipande mbegu hizo hizo kwa misimu 3 ili kudumisha usafi wa aina mbalimbali.

Lima shamba wiki 2–4 za mwanzo wa mvua, na panda wakati wa mvua kwa sababu udongo huwa una maji ambayo huhitajika kwa ukuzaji wa maharagwe.

Acha umbali wa 45cm kati ya mistari na 20cm kati ya mimea. Iwapo unatumia ng'ombe, acha umbali wa 60cm kati ya mistari na 15cm kati ya kulima. Panda mbegu 2 kwa kila shimo.

Ongeza mbolea na uchanganya kabisa na udongo ili kupanua mazao.

Palilia wiki 1–2 baada ya kuota, na baada ya wiki 3 ili kupunguza ushindani wa virutubisho.

Vuna kabla ya maganda kukatika, na tenga maharagwe yaliyokauka na mabichi ili kuepuka hasara.

## **Hatua za baada ya mavuno**

Pura mahargwe kwa upole, juu ya turubai na tenga takataka ili kuhakikisha ubora wa nafaka.

Pepeta ili kuondoa makapi.

Ainisha ili kuondoa mbegu zilizo na kasoro, magonjwa, na kudumisha usafi wa aina mbalimbali.

Chambua mbegu kutegemea rangi, kiwa cha uharibifu, taka, wadudu, na harufu.

Tibu mbegu kwa kutumia kemikali zinazopendekezwa, kwa kipimo kinachofaa. Fungasha na uhifadhi mbegu katika mfuko kwenye mahali pakavu na safi ili kuzilinda dhidi ya wadudu waharibifu.